**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**632** **SAYANSI**

**Muda: Saa3 Hours** **Mwaka: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. (a) Bainisha ugonjwa wenye dalili ya kukojoa mkojo wenye rangi nyekundu baada ya kuoga kwenye bwawa lenye maji yaliyotuama
   (b) Kupendekeza dalili zingine tatu za ugonjwa huo
2. (a) Bainisha tatizo lililompata Amani baada ya kumuona nyoka akikatiza barabarani
   (b) Tumia hoja tatu, kueleza kwa kifupi msaada anaopaswa kupatiwa Amani kabla ya kupelekwa hospitali
3. Chambua kwa kifupi vitu muhimu vinne ambayo huwawezesha ng'ombe na miti kuishi katika mazingira yao
4. Bainisha vigezo vinne vya kuzingatia wakati wa kugawa nishati katika makundi ya nishati jadidifu na zisizo jadidifu
5. Panga simboli za elementi nane katika safu na mistari stahiki kwenye jedwali la mrudio lifuatalo:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | | | | | | | H |
| | | | He | | Ca | | |
| P | | Cl | | | | | Mg |
| | Si | | | | | | |

6. Ainisha mifano nane ya mashine rahisi zenye gurudumu na ekseli zinazopatikana katika mazingira halisi ya mwanafunzi
7. Chambua kwa kifupi mabadiliko manne yatokanayo na balehe kwa wanaume na wanawake
8. Pendekeza mambo manne anayopaswa kufanya mwalimu ili wanafunzi wake wa Sayansi waweze kuchangamka muda wote wa ufundishaji na ujifunzaji
9. Chambua kwa kifupi mambo manne ambayo mkufunzi anatakiwa kuyazingatia kutoka kwa mwanachuo anayefundisha wanachuo wenzake
10. Thibitisha kauli ifuatayo kwa kutoa hoja nne. "Kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia kutoka kwenye mazingira halisi ni muhimu sana shuleni."

**SEHEMU B (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. (a) Chora mchoro utakaotumika katika kuunda sakiti ya umeme kwa kuzingatia vifaa vifuatavyo; waya, swichi, seli kavu, glopu, voltimita na amita
    (b) Onesha kazi ya kila kifaa katika sakiti ya umeme iliyoundwa
    (c) Bainisha vifaa vingine viwili vinavyoweza kutumika kama kikinza umeme akiacha waya na glopu
    (d) Eleza kwa kifupi namna sakiti hiyo inavyofanya kazi
    (e) Ikiwa tofauti ya potenshali kati ya ncha za waya uliotumika ni voti 12, waya huo utakuwa na ukinzani wa Ohm ngapi kama kiasi cha mkondo wa umeme unaopita katika sakiti hiyo ni ampia 0.4?
12. Thibitisha usemi ufuatao kwa kutoa hoja sita. "Mwili wa binadamu umeundwa kwa mifupa mbalimbali ambayo hufanya kazi kwa pamoja katika kuhakikisha binadamu anaendelea kuishi."


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

13. Eleza kwa ufasaha vipengele sita vitakavyotumika katika kuwaongoza wanafunzi kufanya uchunguzi wa kisayansi ili kubaini tabia za maada zenye tindikali kwa kutumia karatasi ya litimasi
14. Eleza sababu sita zinazomfanya mwalimu kusahihisha daftari za wanafunzi wake baada ya kutoa zoezi darasani


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org